**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**NAMBA ZA SIMU**

Mkuu wa Shule- 0756015658

M/ Mkuu wa Shule- 0763685895/0628033907

Patron -0766230585

Mhasibu - 0753760283

Shule ya Sekondari Lupembe

S.L.P 114- NJOMBE

Tarehe 14/06/2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE HALMASHAURI YA NJOMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2023**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya CBG/EGM

Shule ya Sekondari LUPEMBE ipo umbali wa Kilometa 70 Mashariki mwa Mji wa NJOMBE Usafiri wa basi ni **TSHS 6,000/=** kutoka stendi kuu Njombe mjini hadi shule ilipo.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 13/8/2023** Mwisho wa kuripoti ni **tarehe 31/08/2023**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**

**1. SARE ZA SHULE**

i. Suruali 2 rangi ya kijivu mpauko zenye mifuko 2 mbele na 1 nyuma, upana miguu. inch.18 na tai rangi nyeusi.

ii. T-shirt2 za rangi ya kijivu mpauko zenye kola (form six);

iii. Sweta 2 rangi ya kijani jeshi. Track suit rangi kijivu., Mashati meupe 2 ya mikono mirefu.¬

iv. Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu.

v. Raba nyeusi, jezi nyekundu isiyo na maandishi na track suit rangi nyekundu kwa, ajili ya michezo(muhimu sana) Soksi jozi 4 au zaidi rangi nyeusi na soksi nyekundu za michezo pair 2.

v. Koti jeupe lenye mikono mirefu (laboratory coat) kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi tu.

vi. Suruali nyeusi 2 za kitambaa, ambayo ni sare ya kazi baada ya masomo.

**2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni**

i. Ream ya karatasi 2 A4(kwa mwaka)

ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(orodha imeambatanishwa)

iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa biology

iv. Scientific calculator original

v. Godoro la ft.21/ 2

vi. Mashuka 2 rangi light blue,blanketi 1,foronya na mto.

vii. Vyombo vya chakula(sahani,bakuli,kikombe na kijiko)

viii. Vifaa vya usafi na kazi za nje.

**CBG** Aje na Shoka lenye mpini, ndoo mbili kwa ajili ya usafi moja lita 20, nyingine ya lita 10 na soft bloom.

**EGM** aje na panga, mopa, Ndoo mbili kwa ajili ya usafi moja lita 20, nyingine ya lita 10 na soft bloom.

ix. Tochi kwa matumizi binafsi nyakati za usiku ni muhimu sana (ingawa umeme upo)

x. Aje na bima ya afya,cheti cha kuzaliwa na result slip pamoja na folder file moja.

xi. Madaftari makubwa 10 (counter book Q3) au zaidi, pen, penseli,rula na mkebe.

xii. Toilet paper za kutosha muhula mzima.

Aidha mshono ufanane na sare ya darasani.

Tanibihi: 1. Kuepusha usumbufu vitu vifuatavyo vinapatikana mazingira jirani na shule;

(Tshirt kijivu, Tai, sweta, nguo za michezo, mashati meupe ya shule, soksi nyeusi, raba za michezo, mashuka)

.

**3.MICHANGO MBALIMBALI**

Michango yote italipwa kupitia akaunti namba 60601000014 NMB BANK Jina la akaunti LUPEMBE SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTI.

Tafadhari andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip.Pindi afikapo shuleni aiwasilishe hati ya malipo kwa mhasibu wa shule.

Mchanganuo wa michango ya Shule upo kwenye jedwali hapo chini

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**4.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**5. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

***N.B Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**6. BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI:**

1.Jina la mwanafunzi……………………………………………………………….

2.Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………

3.Mahali alipozaliwa(wilaya)…………………. (mkoa)…………………………

4. Dini……………………….... Dhehebu………………………………………….

5.Jina la mzazi/mlezi anayekutunza………………………………………………. .Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………………………….. .Anwani ya mzazi/mlezi………………………………………………………….NO ya simu………………………….

6.. Mahali anapoishi mzazi/mlezi: -mkoa………………wilaya……………………. Kijiji/mji……………………………….kata……………………………………….. .Jina la anaye kulipia michango ya shule………….........................uhusiano…………………… .Anwani yake……………………………………………………………… 3.Namba ya simu…………………………………………………………..

5. Anwani za ofisi ya katibu kata au mwenyekiti wa mtaa/kijiji ambako mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaishi:- .Jina la kata…………………………………………………………………..
.Anwani……………………………………………………………………………….
.Namba ya simu……………………………………………………………………… .Jina la mwenyekiti wa kijiji/mtaa………………………………………………….... .Kijiji/mtaa wa ………………………………………………………………………
3.Anwani…………………………………………………………………………………
4.Namba ya simu…………………… 1

.Jina la ndugu wa karibu…………………………………………………..................
2.Kijiji/mtaa wa ………………………………………………………………………
3.Anwani…………………………………………………………………………………
4.Namba zake za simu………………………………………………………………………

7. **FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.**

I. MWANAFUNZI Mimi…………………………………………….kidato ………….
Nakubali kujiunga na shule hii ya sekondari Lupembe nikiwa mwanafunzi wa Bweni.Nimesoma na kuyaelewa maelezo yote, sheria na taratibu zote za shule.Ninakubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Lupembe.Kwa hiyo ninaahidi kwamba :- 1.Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu. 2.Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa chama tawala na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 3.Nitatunza mali ya uma ambayo ni pamoja na mazingira, samani, vitabu nk. 4.Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu. 5.Nitashiriki katika shughuli nyingine za nje mbali na masomo ya darasani. Sahihi ya mwanafunzi……………………….
Tarehe………………………

II. MZAZI/MLEZI: Mimi……………………………………..ninakubali mtoto wangu………………......................... kujiunga shule ya sekondari Lupembe kidato…………mwaka 2023/2024 tarehe………….akiwa mwanafunzi wa bweni.Kwa hiyo naahidi kwamba :- 1.Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wengine wa shule katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu.Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu. 2.Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulukwa muda wote awapo shuleni.
Anwani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………………………
Namba ya simu ya mzazi/mlezi…………………………. Email…………………………………
Sahihi ya mzazi/mlezi……………..……tarehe…………………….

**8. FOMU YA KUPIMA AFYA YA WWANAFUNZI LUPEMBE SECONDARY SCHOOL, P.O.BOX. 114, NJOMBE.**

DATE:………………………….. THE MEDICAL OFFICER:
……………………………………….. ………………………………………
………………………………………. RE:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION To be completed by a medical officer in respect of all form five students Full name…………………………………age………….……….years. Sex……….

1. Blood count(red and white)………………………………………………………...

2. Stool examination…………………………………………………………………..…

3. Urine analysis………………………………………………………………………

4. Eye test……………………………………………………………………………..

5. T.B test……………………………………………………………..…………………

6. Ears…………………………………………………………………………………

7. Chest…………………………………………………………………………………..

8. Spleen………………………………………………………………………………

9. Abdomen………………………………………………………..……………………

10. ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical defects or important infections, chronicof family diseases etc.
………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

11. General comments:-
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
SIGNATURE…………………………… DATE……………...….STAMP

**9. ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILASOMO**

**A: CHEMISTRY**

Advanced chemistry Review by Willam W Davis(Mzumbe bookshop project 2004)

Physical chemistry by Delungu et(Mzumbe bookshop project 1998)

Advanced level in organic chemistry part I and II(TIE 1995)

Organic chemistry volume I.The fundamental principles by I.L Finar(Longman Ltd 1990)

NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY PHYSICAL CHEMISTRY 2014

NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY ORGANIC CHEMISTRY 2014

NGAIZA'S SERIES OF ADVANCED CHEMISTRY INORGANIC CHEMISTRY 2014

B: BIOLOGY New understanding Biology by Suzan Tool

Advanced biology by Michael Kent

Biological science third by D.J.Tylor, N.P.O Green and G.W.Stout

Advanced biology principle and applicationby C.J.Clegg and D.G.McKean

New understanding biology for advanced level by Glenn and Suzan Tool

Plant and animal biology vol.1•&2 by A.E. Vines and N.Rees Biology for class XI&XII by Dr.P.S.Verma and Dr. B.P.Pandey Biological science by CHANDS

Biology by Msaki series (classification, genetics and cytology)

**C: GEOGRAPHY**

Principle of physical geography by F.J.Monkhouse•

Geography;Integrated Approach by D.Waugh•

Practical geography for Africa by J.M.Pritchard•

General geography in diagram by R.B.Bunnert•

Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita•

Simplified physical geography(A level) by D.M•

Statistical methods and the geographers•

Human and Economic Geography by Morgan goh cheng leong•

**D: ADVANCED MATHEMATICS.**

CHANDI I• & II  BACKHOUSE I• & II  PURE MATHEMATICS I• & II

UNDERSTANDING ADVANCED MATHEMATICS•

ENGENEERING MATHEMATICS•

PURE MATHEMATICS ( TRANTER)•

REVIEWS ADVANCED MATHEMATICS 1• & 2  KINUNDA•  UNDERSTANDING MATHEMATICS•

**D: BASIC APPLIED MATHEMATICS**

Basic Applied Mathematics by Kiza and Septine I.Sillem•  Basic Applied Mathematics by TIE

Pure mathematics I•&II by Bank house  Core course Mathematics by Bostoch and Chandler

**E:ECONOMICS**

MORDEN ECONOMIC –ROBERT MUDIDA•

ECONOMIC 1 ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS•

ECONOMIC 1I ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS•

ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1 AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE NEW•

SYLABUS  ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1I AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE• NEW SYLABUS

ESSENTIALS FOR A LEVEL ECONOMICS PAPER 1 FORM 5&6 BY  AMBROSS ODHIAMBO

ESSENTIALS FOR A LEVEL ECONOMICS PAPER 1 FORM 5&6 BY  AMBROSS ODHIAMBO

**F. GENERAL STUDIES**

General studies for A-Level certificate form v•

Contemporary approach for A-level general studies•

notes for form five and six  General studies supplementary book for A level and colleges•

Advanced level general studies notes for form 5 and 6 by Nyambari Nyangwine 2009•

General studies for A-Level certificate form v and vi by Richard R.F.•

NB MWANAFUNZI LAZIMA AWE NA KITABU KIMOJAWAPO KWA KILA SOMO LA TAHASUSI YAKE. SIMU HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule .JOSEPHINA A. KAZIULAYA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0756015658.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0628033907/0763685895**
- **Mwandamizi Taaluma 0754-231771**
- **Mwandamizi Malezi 0743271823/0673201823**